

Na Fadhil Rashid, Kilosa

Wafanyabiashara wanaonunua mazao kwa wakulima wilayani Kilosa wamepigwa marufuku kujaza zaidi ya ujazo wa kawaida kwa kushonea viremba kwenye maguania maarufu kwa jina la lumbesa na atakayekaidi agizo hilo serikali haitamvumilia.

Agizo hilo limetolewa Septemba 21 mwaka huu na Mkuu wa Mkoa Morogoro Kebwe Steven Kebwe kwenye kijiji cha Lumuma wilayani Kilosa alipokuwa akiongea na wananchi wa kijiji hicho wakati wa mkutano wa hadhara alipokuwa kwenye ziara ya siku tatu wilayani Kilosa.

Kebwe amesema sheria za nchi zinakataza kujaza gunia kwa kushonea kiremba badala yake gunia litakiwa kupimwa kwenye mzani na wale wanaoshonea na viremba wanafanya makosa ya kukwepa ushuru wa serikali kinyume cha sheria na pia gunia kulifanya kuwa kubwa kwa mmbebaji hivyo kuhatarisha afya za nguvu kazi ya taifa wanaobeba gunia hilo.

Aidha kwenye ziara hiyo mkuu huyo wa mkoa aliweza kuyakuta magunia ya vitunguu yakiwa tayari kwa kusafirishwa ya wafanyabiashara kwenye kata ya Lumuma na Kidete yakiwa yameshonwa kinyume cha sheria kwa kuwekwa viremba ambapo aliwaamuru kufumua magunia yote na kuondoa viremba na kushona mshono unaojulikana kwa jina la zipu ambao unakubalika na serikali.

Kwa upande mwingine Kebwe amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Ndugu Kessy Mkambala kuhakikisha hakuna mfanyabishara anayenunua mazao wilayani Kilosa kwa kushona viremba na watakaokaidi awachukulie hatua za kisheria wakati huo huo amemtaka kutenga fedha kwa ajili ya kujenga soko la mazao kwenye kijiji cha Lumuma ili wafanyabishara hao kwenda kununua mazao kwenye soko hilo tofauti na sasa wananunua kiholela na kusababisha wafanyabishara wengi kukwepa kutoa ushuru hivyo kuikosha mapato Halmashauri hiyo.